

# Kusaidia Maelekezo ya Mazingira ya Mtoto Wako katika Elimu ya Awali na Huduma za Malezi

KISWAHILI

Mwanzo mzuri wa elimu ya awali ni muhimu. Ni muhimu wewe na familia yako mhisi mmekaribishwa, salama na mnaungwa mkono. Siku za kwanza kwenye huduma zinahusu mtoto wako kuwafahamu watoto wengine na kuanza uhusiano wa kuaminiana na walimu, waelimishaji na wataalam wengine wa watoto wadogo.

Elimu ya Awali na Huduma za Malezi katika Jiji la Victoria zinaongozwa na *Mfumo wa Kujifunza na Maendeleo ya Watoto Wadogo Victoria* (Victorian Early Years Learning and Development Framework) (VEYLDF). Mfumo huu unawajulisha waelimishaji kwamba utambulisho wa watoto na familia zao na historia za utamaduni zinarekebisha ujifunzaji na maendeleo yao. Watoto wanahisi kukaribishwa na wanajifunza vizuri pale wataalam wanapohesimu na kukubali utambulisho wao wa kipekee' (VEYLDF, 2016, pg. 12). Uelewa huu utajikita katika mbinu ambayo waelimishaji watatumia wakati wa kukusaidia wewe na mtoto wako katika kipindi cha maelekezo ya mazingira na upangaji katika Elimu yao ya Awali na Huduma ya Malezi.

Elimu ya Awali na Huduma za Utunzaji hutazama ushirikiano shirikishi kati ya waelimishaji na familia kama msingi wa mpango bora. Uhusiano wa heshima kuanzia mwanzo ni kiashiria thabiti cha huduma ya hali ya juu. Unaweza kutarajia waelimishaji kuwa wachangamfu na wanakaribisha na kuhimiza matumizi ya lugha ya familia yako.

Huduma zinaweza kusaidia mawasiliano nawe kupitia huduma ya mkalimani kwa nja ya simu ili kuhakikisha kuwa umefahamishwa ipasavyo na una fursa ya kuuliza maswali na kutafuta taarifa zaidi katika lugha unayoifurahia zaidi. Aidha, mfanyakazi wa msaada ambaye anazungumza lugha ya familia yako anaweza kupatikana ili kumsaidia mtoto wako kwa muda mfupi kadri anapokuza mahusiano na hisia ya kuhusika katika huduma.

Elimu ya Ubora ya Awali inatambua familia kama 'ushawishi wa msingi katika ujifunzaji na maendeleo ya watoto' (VEYLDF, 2016, pg. 9). Waelimishaji wanathamini na kutafuta mchango na ushiriki wa familia katika mpango wa watoto wadogo. Hii haielezi tu utendaji wa waelimishaji lakini pia huwasaidia watoto kukuza uaminifu, usalama na uhusiano kati ya watu katika mazingira yao ya elimu na malezi na mazingira ya nyumbani ambayo huongeza matokeo ya kujifunza. Pia familia zinahimizwa kushiriki kwenye huduma na kuhudhuria katika vipindi vya awali. Hili humsaidia mtoto wako kujisikia salama na kukusaidia kuelewa kinachotokea kwenye huduma pale mtoto wako anapokuwa hapo bila uwepo wako.

Huduma yako ya elimu ya awali itakuwa na mpango wa maelekezo ya mazingira ili kukusaidia wewe na mtoto wako kuwa na uelewa wa huduma. Hii inaweza kujumuisha;

- kutembelea huduma na mtoto wako kabla ya mahudhurio rasmi kuanza
- kuanza na vipindi vifupi na kuongeza vipindi virefu zaidi ili kukusaidia wewe na mtoto wako kujisikia vizuri.

*fka* Children's Services
18 Harper Street, Abbotsford VIC 3067

03 9428 4471 | fkacs@fka.org.au
www.fka.org.au | Facebook @FKACS

Waelimishaji wako wa elimu ya awali watajumuika na wewe na watakuuliza maswali kadhaa kuhusu wewe na mtoto wako. Hii itawapa uelewa mzuri wa mahitaji ya mtoto wako na kumsaidia kuunda mpango ambao huongeza fursa za kujifunza na matokeo chanya kwa mtoto wako.

Mifano ya maelezo ambayo huduma za watoto wadogo wanaweza kukuomba uwaeleze ni;

- Taarifa kuhusu afya ya watoto - kumbukumbu za chanjo, mahitaji ya matibabu, magonjwa au mizio.
- Upendeleo wa kubadili nepi, upendeleo wa kwenda choo na mazoea ya nyumbani.
- Vyakula ambavyo watoto hula, desturi/taratibu za wakati wa chakula.
- Mahitaji ya mtoto kupumzika/kulala.
  - Je, wanalala kwenye kitanda cha mtoto, kitanda chao wenyewe au wanalala pamoja na wengine?
  - Ni nyimbo gani zinaweza kuwafariji?
  - Je, wana kitabu wanachokipenda, mwanasesere au blanketi maalum?
  - Kwa kawaida huwa wanapumzika/wanalala saa ngapi mchana?
- Je, sherehe na mila gani ni muhimu kwa familia yako?
- Waelimishaji watapokea taarifa nyingine yoyote ambayo ungependa kuwaeleza.
- Pia utakuwa na taarifa kuhusu mtoto wako ambayo ungependa Waelimishaji waifahamu ambayo itamsaidia wakati wa kumhudumia mtoto wako.

## Njia zingine za kumsaidia mtoto wako anapokuwa ametulia katika huduma yake ya utotoni

- Jumuika na mtoto wako kwenye huduma - mweleze mtoto wako taratibu za huduma, cheza, soma hadithi na imba nyimbo katika lugha yako mwenyewe.
- Wasaidie kuwasiliana na watoto wengine. Hii inaweza kuwa kwa kuwahimiza kuketi karibu na wengine, kujitambulisha kwa watoto wengine, kujiunga katika shughuli na michezo.
- Jumuika kuzungumza na mtoto wako pamoja na watu wengine wanaozungumza lugha moja.
- Zungumza na mtoto wako kuhusu kile anachopitia na anachohisi: watie moyo.
- Hakikisha mtoto wako anawajua waelimishaji wake ni akina nani, majina yao na kwamba anaweza kwenda kwao ikiwa atahitaji msaada wowote. Wape fursa ya kufanya mazoezi ya kutaja majina ya muelimishaji wao mkishirikiana na muigie mkiomba usaidizi.
- Kila mara waage kabla ya kuondoka na umhakikishie mtoto wako kuwa utarudi baadaye. Ni wazo zuri kumtuliza mtoto wako kwa kumsaidia kushiriki katika shughuli na mwalimu na/au watoto wengine kabla hujaondoka.
- Jadili taratibu na mazingira ya huduma na watoto usiku/asubuhi kabla ya kuhudhuria ili kuwapa fursa ya kuuliza maswali yoyote na wewe kujibu masuala yoyote wanayoweza kuwa nayo.
- Kumbuka walimu na waelimishaji wa mtoto wako wapo pale kukusaidia wewe na mtoto wako mnapokuwa kwenye huduma.

**Marejeo**

Department of Education and Training, 2016. *Victorian Early Years Learning and Development Framework*.